



Unachohitaji Kujua Kuhusu kuvalia barakoa Minnesota Masharti ya kuvalia barakoa (kifunika uso)

Watu wote wanaioishi Minnesota wanatakiwa kuvalia Barakoa (kifunika uso) wanapokuwa katika biashara zote za ndani na pia kwenye maeneo yote ya ndani ya uma, isipokuwa ukiwa peke yako. Wafanyikazi pia wanalazimika kuvalia barakoa wakiwa nje wakati ambapo ni vigumu kudumisha umbali. Ni jambo la muhimu kujua yanayohitajika.

Ni jambo la muhimu sana kuzingatia umbali wa futi 6 kwa watu usioishi nao hata ikiwa umevalia barakoa (kifunika uso). Kila mtu anapaswa kuendelea kuosha mikono yake mara kwa mara na kukaa nyumbani akiwa mgonjwa.

Wakati unapostahili kuvalia barakoa (Kifunika uso)

- Katika biashara zote za ndani na sehemu zote za uma za ndani, ikiwa ni pamoja na wakati wa kungojea nje ili kuingia kwenye sehemu za ndani za uma au za kibiashara.
- Wafanyikazi wote pia wanalazimika kuvaa kifunika uso wanapokuwa nje ikiwa hawawezi kuzingatia umbali wa futi 6 kati ya watu.
- Unaposafiri kwenye vyombo vya usafiri wa uma kama vile mabasi au gari moshi, au kwenye teksi, ama kwenye gari linalowabeba watu wengi, au gari linalotumika kwa sababu ya biashara.
- Biashara zingine aidha ziwe za ndani au za nje zinaweza kuwa na sheria zaidi kuhusu wakati unapohitajika kuvalia barakoa (kifunika uso). Ni lazima ufuata maagizo hayo.

Aina za Barakoa (Kifunika uso)

- Aina za barakoa (vifuniko vya pua na mdomo) vinaweza kujumuisha karatasi au maski inayoweza kutolewa, Maski ya kitambaa, kinga shingo, skafu, bandana au vifuniko vya uso vya kidini.
- Barakoa lazima zifunike pua na mdomo kabisa. Barakoa hazifai kubana sana lakini inapaswa kuvalika vizuri.
- Usivalie barakoa zilizo na valvu au vipumulio vingine. Hii inaweza kuruhusu matone ambayo hubeba virusi kutoka nje.
- Hupaswi kuvaa maski za upasuaji au vifaa au vipumuzi vya N95 isipokuwa unazihitaji kwa sababu ya kazi yako.
- Kwa maelezo zaidi kuhusu kwa nini barakoa ni muhimu na jinsi ya kuvaa kwa usahihi, nenda kwa Maski na vifunika uso (www.health.state.mn.us/diseases/coronavirus/prevention.html#masks).

Watu ambao hawahitajiki kuvalia barakoa

- Watoto chini ya umri wa miaka 2 hawapaswi kuvaa barakoa (kifunika uso).
- Watoto wa kati ya umri wa miaka 2 hadi 5 hawatakiwi kuvalia barakoa, lakini ikiwezekana wanahimizwa wavae wakiwa kwenye maeneo ya uma.
- Watu walio na shida za kiafya, ulemavu au afya ya kiakili, au upungufu wa akili ambao utawafanya kuwa vigumu kuvumilia barakoa.
- Mtu yeyote ambaye ana shida ya kupumua, amepoteza fahamu, amelala, hajiwezi, au asiyekuwa na uwezo wa kuondoa barakoa bila kusaidiwa.
- Aina nyingine za maski kama vile vifunika uso wote vinaweza kuzingatiwa kwa wale walio na hali duni ya kiafya au hali ambayo haiwezekani kuvalia maski.

Wakati barakoa inapoweza kutolewa kwa muda

Barakoa inaweza kutolewa kwa muda mfupi. Hizi ndizo nyakati ambazo barakoa inaweza kutolewa, lakini unaweza kupata orodha kamili kuhusu kuvalia barakoa na mapendekezo ya Agizo la Utendaji 20-81 (www.health.state.mn.us/diseases/coronavirus/facecover.html).

- Wakati unapokula au kunywa, unaweza kukaa umbali wa futi 6 kutoka kwa watu wasio wa jamii yako.
- Wakati unapohitajika kuonyesha kitambulisho chako wakati wa kuagiza vinywaji kama vileo au unapoingia sehemu fulani.
- Wakati wa kuogelea au kufanya shughuli nyingine ambapo barakoa itapata kuwa majimaji
- Wakati unapowasiliana na mtu ambaye ni kiziwi au ana ugumu wa kusikia, au ambaye ana hali pungufu ya ulemavu, au unapowasiliano na mtu mwenye akili punguani ambaye hatakuielewa wakati amevalia maski. Unapaswa kukaa umbali wa futi 6 kutoka kwa mtu huyo.
- Wakati unaposhiriki katika michezo au mazoezi ya viungo ambapo unapumua sana na kuvalia barakoa ni vigumu.

UJUMBE ZAIDI KUHUSU KUVALIA BARAKOA (KIFUNIKA USO)

Kwa habari zaidi kuhusu Agizo la Utendaji, pamoja na sheria maalum za viwanda (kama vile, utunzaji wa kibinafsi, shule, na utunzaji wa watoto), adhabu na utekelezaji, na mahitaji ya biashara, tazama:

- Tazama Agizo la Utendaji 20-81 linapatikana katika Maagizo ya Utendaji kutoka kwa Gavana Walz (<https://mn.gov/governor/news/executiveorders.jsp>).
- Maswali yanayoulizwa mara kwa mara kuhusu mahitaji ya kuvalia barakoa (Kifunika uso) (<https://www.health.state.mn.us/diseases/coronavirus/facecoverfaq.html>)



Idara ya afya Minnesota | health.mn.gov | 651-201-5000
625 Robert Street North PO Box 64975, St. Paul, MN 55164-0975
Wasiliana kwenye health.communications@state.mn.us kuomba njia mbadala.

08/06/2020 (Swahili)

Ukurasa 2 kati ya 2